ERETO - NGORONGORO PASTORALIST PROJECT

RIPOTI YA WARSHA

Warsha Shirikishaji ya kuandaa Mipango
ya
Ereto – Mradi wa Wafugaji Ngorongoro

5 - 7 Oktober 2000

Mwezeshaji - Loserian Sangale

1.0 UTANGULIZI

1.1 MRADI WA ERETO

Ushauri huu uliagizwa na Ubalozi wa Falme ya Denmark kuandaa Warsha ya kushirikiana kuhusu Mradi wa wafugaji wa Ngorongoro (Ereto – NPP) ulioko katika eneo la Hifadhi ya Ngorongoro (NCA). Mradi huu unahusisha Serikali mbili, ya Tanzania na ya Denmark. Madhumuni ya mradi huu ni kuyashughulikia matatizo makubwa yanayohusu ufugaji katika eneo la Hifadhi. Tatizo la kwanza kabisa ni afya ya mifugo, likifuatiwa na umasikini, hali mbovu ya miundo mbinu ya usambazaji wa maji na kupungua kwa upatikanaji wa malisho. Mradi huu unagharamiwa na Shirika la Maendeleo la Kimataifa la Denmark (DANIDA), Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro (NCAA) na wafugaji waishio kwenye Hifadhi na unategemewa kufanyika kwa miaka mitano katika awamu mbili. Awamu ya Kwanza ilianza Julai, 1998 na kuishia Desemba, 2000. Awamu ya Pili itaanza Januari, 2001.

Kwa vile awamu ya kwanza inakaribia kwisha, matayarisho kwa ajili ya shughuli za Awamu ya Pili yameshaanza. Hii ni pamoja na kuwasiliana na washiriki muhimu katika Mradi. Madhumuni ya Warsha hii ni kuwashirikisha wahusika wote wa Mradi katika kupanga Awamu ya Pili ya Mradi wa Wafugaji wanaoishi katika Hifadhi ya Ngorongoro kwa njia ya Warsha ya LFA. Kwa hiyo Warsha hii ni sehemu moja muhimu ya kupeana mawazo. Inahusisha uchangiaji wa mawazo miongoni mwa washiriki wakiwa ni pamoja na Ilaigwanak ambao ni viongozi wa jadi, wawakilishi wa Kamati za Ewoloto, wanawake viongozi wawakilishi katika serekali za mitaa na watumishi wa Mradi. Warsha hii ilihudhuriwa na jumla ya washirki 39 (tazama kiambatanisho 1) na ilifanyika kuanzia tarehe 5 hadi 7 Oktoba pale Ngorongoro (tazama kiambatanisho 2).

Mwenendo wa Warsha

Warsha ilifunguliwa rasmi na Meneja wa Mradi, Bwana M. Nasei ambaye aliwakaribisha washiriki wote kwa moyo mkunjufu. Alieleza madhumuni ya warsha na katika kusaidia kulizungusha gurudumu la warsha, aliendelea kwa kutoa ujumla wa kutekelezaji wa sehemu mbali mbali za mradi katika kipindi cha mwaka mmoja na nusu uliopita. Hii ilisaidia kuwafanya washiriki kuwa na mwangalio mzuri na hivyo kuwako kwa msingi unaofaa kwa ajili ya zoezi la mpango. Baada ya hapo alimkabidhi mwendesha warsha Bwana Loserian Sangale shughuli za warsha.

Kiwango cha elimu mongoni mwa washiriki wa warsha kilitofautiana kwa kiasi kikubwa, wakiwepo wachache wasiojua kusoma na kuandika na hata kuelewa Kiswahili vizuri. Walikuwepo vile vile wengi wenye elimu ya msingi na ya sekondari na wachache wenye stashahada na shahada. Kutokana na hali hii, ilibidi mwendesha warsha atumie lugha ya Kimaasai na ya Kiingereza. Aidha, ilimaanisha kuwa mawazo ya muundo wa mantiki lazima yatolewe kwa makini ili kuhakikisha kuwa washiriki wote wanaelewa na kuchangia. Hivyo basi, mantiki ya mradi huu ilijadiliwa kwa kutumia michoro tofauti, mchoro mmoja wa matatizo na mwingine wa madhumuni, na vile vile kwa njia ya uchambuzi wa wenye maslahi husika. Kisha kuliangalia kwa nia na madhumuni ya sasa hivi kama ilivyopangwa na tuliendelea kuchambua utekelezaji wake. Hii iliwawezesha washiriki kuyatambua maeneo yatakayohitaji kuboreshwa katika Awamu ya Pili. Sehemu ya mwisho ya warsha ilijaribu kuchangia katika kutunga videkezo ambavyo inatumainika kuwa baada ya kuchujwa vitatumiwa katika Awamu ya Pili.

Madhumuni ya Warsha

(a) Maandalizi ya Awamu ya Pili ya Mradi baada ya kumaliza Awamu ya Kwanza.

(b) Kutathmini mafanikio ya Mradi hadi sasa.

(c) Kupima maeneo katika Mradi ambayo utekelezaji wake ni dhaifu na kutafakari namna ya kuyaboresha.

(d) Kutoa mawazo na mapendekezo yatakayotumiwa na ujumbe wa Denmark ambao utakuja kumalizia utungaji wa Awamu ya Pili ya Mradi wa Wafugaji Ngorongoro.

(e) Kushirikisha kikundi kilicholengwa katika utengenezaji wa maandishi ya Awamu ya Pili ya Mradi.

2.0 MTAZAMO WA JUMLA WA UTEKELEZAJI KATIKA AWAMU YA KWANZA - Yaliyo Muhimu

Tathmini ilifanyika kuhusu mafanikio ya utekelezaji katika sehemu kuu tano za programu. Toleo hili linaangalia kilichopangwa na kilichotekelezwa kama ifuatavyo:

2.1 Programu ya Jamii – EWOLOTO

Mpango: Nia ya sehemu hii ni kupunguza umasikini kutokana na mgao wa mifugo katika jamii, hii huitwa ewoloto. Uhamisho huo wa

mifugo kuelekea kwa masikini umesaidiwa pia kwa kugawiwa nafaka na kupatahuduma za mifugo kwa familia hizo zinazopewa mifugo. Lengo lilikuwa Mradi uweze kusaidia familia zipatazo 3,400 kwa kuipatia kila familia kiwango cha chini cha mifugo 9 katika kipindi cha miaka minne.

Utekelezaji: Jumla ya familia 1,857 (ambayo ni 54.6% ya Lengo) zimenufaishwa na Mradi. Jumla ya familia 1,543 (ambayo ni 45.4%) bado hazijapata mifugo, lengo ambalo litatekelezwa katika kipindi kilichobaki.

2.2 Upatikanaji wa Maji na Menejimenti ya Renji

Mpango: Mpango ulikuwa kuzisaidia jamii katika msingi wa kushirikiana gharama kukarabati mfumo wa upatikanaji wa maji na kutengeneza mingine mipya. Washauri wahandisi walikwisha tayarisha mipango ya kutengeneza malambo 5 na ya ukarabati wa mengine 2. Kazi za uchimbaji wa visima, mashimo ya maji na uendelezaji wa maeneo yenye majabali yenye uwezo wa kuhifadhi maji na usambazaji wa maji kwa mabomba zimefanyika. Mradi pia utazisaidia jamii kutengeneza mipango ya matumizi ya ardhi inayounganisha maji na malisho na mambo mengine yanayohusiana na matumizi ya ardhi.

Utekelezaji: Shughuli za maendelezi ya maji ziko katika hatua mbali mbali za utekelezaji zikiwemo zile zilzokwisha kamilika, kazi za ujenzi ambazo bado zinaendelea na zile ziliziko katika hatua za upimaji. Hadi sasa, ujenzi wa malambo 2 na mashimo ya maji 2 umekamilika wakati ujenzi wa malambo ERETO na mashimo ya maji ERETO bado unaendelea. Kamati za maji zimekwisha undwa katika jamii zote.

2.3. Mgao wa Mahindi:

Mpango: Ili kusaidia programu za jamii, mradi ulitazamiwa kumpatia kila mlengwa kilo 45 za mahindi kila mwezi kwa miaka 3.

Utekelezaji: Ugawaji wa mahindi uliendelea vizuri hadi mwezi Machi 2000. Baada ya hapo ugawaji haukuwa wa kuaminika kwa sababu kiasi kilichokuwa kinagawiwa kilikuwa cha chini mno kuliko kiwango kilichokubaliwa na miezi mengine hapakuwa na mahindi kabisa. Upungufu ulijitokeza hasa katika miezi ya Aprili, Mei, Juni na Julai. Bajeti iliyopangwa iliathiriwa sana na kupanda kwa bei ya mahindi iliyosababishwa na mavuno duni katika msimu huu wa kilimo.

Huduma za Mifugo

Mantiki ya madhumuni ilikuwa kwamba upatikanaji sahihi wa huduma za mifugo pamoja na mafunzo ya wafugaji yatapunguza vifo vya mifugo na hivyo kuchangia katika upatikanaji wa mifugo watakaohitajika katika programu ya jamii.

Mpango: Kuwapatia wafugaji huduma za bure za mifugo kwa muda wa miaka miwili kwa kupitia kwa wataalamu mifugo binafsi. Wataalamu wa mifugo wangewafunza watu wawili waliochaguliwa kutoka kila kijiji, jinsi ya kutibu magonjwa yanayotokea mara kwa mara.

Uteklezaji: Huduma za mifugo zinatolewa kwa wanafamila 1,857 wa ewoloto kwa kupitia kwa wataalamu wa mifugo ambao wamewekeana saini mkataba na Mradi. Wataalamu hurudishiwa gharama zao. Kadhalika wataalamu hutoa huduma kwa wanajamii wengine, ambao hulipia huduma hizo wenyewe.

Menejimenti ya Mradi:

Dhana ya maandishi ya Mradi ilikuwa “Mradi utatekelezwa chini ya PIU ikiwa chini ya Kamati ya Uendeshaji ambamo kutakuwepo wawakilishaji kutoka Baraza la Wafugaji na ujumbe wa NCAA na kwamba wajumbe wote wa PC waliochaguliwa watapewa mafunzo katika mbinu za menejimenti”.

Utekelezaji: Mafunzo kuhusu uongozi na sheria za ardhi yameishatolewa kwa wawakilishi wa jamii.

3.0 KUCHUNGUZA MANTIKI YA MRADI:

3.1 Mti wa tatizo na Mti wa lengo: Hii ilihusisha kuupa mtazamo tena mti wa tatizo kama ulivyotolewa katika maandishi ya Mradi. Washiriki walichunguza kwa makini tatizo kubwa ambalo ni hali ya umaskini mkubwa ambayo inaendelea kuwakabili wafugaji katika NCA na kutafuta ni sababu zipi zinazochangia hali hiyo (tazama kielelezo 1), waliafiki mantiki kama ilivyo kwenye mti wa tatizo. Kisha walizungumzia mti wa lengo, sababu muhimu ikiwa kuboresha maisha ya wafugaji katika NCA na kimsingi kukubaliana na mantiki ya mchoro.

Washiriki walichukua muda katika kuchunguza sehemu ya juu ya mti wa tatizo ambao ni matokeo ya tatizo kwa vile sehemu hiyo yaonekana kutokuzungumziwa sana katika maaandishi ya Mradi. Matokeo mbalimbali ya tatizo yalichunguzwa na kuongezwa katika sehemu ya

juu ya mti wa tatizo. Haya yatachangia kwenye mazungumzo ya vielelezo na msukumo wa Mradi kuhusu tatizo.

3.2. Uchambuzi wa wenye maslahi: Washiriki pia walitaka kujua nani washika dau kwenye Mradi na maslahi yao na umuhimu wa Mradi kwao na mchango wao kwenye Mradi. Hayo yalikuwa mambo muhimu na yalielezea mchango wa kila moja kwenye Mradi pamoja na uwezekano wa athari kutoka kwa baadhi ya wenye maslahi (tazama kielelezo 2).

KIELELEZO 1:

Mchoro wa Matatizo ya Eroto – Mradi wa Wafugaji Ngorongoro

Jamii ina dhoofu	
Jamii inakuwa dhoofu	Vifo
Kuteseka hatimaye vifo	Kudhoofu mwili na maradhi
Kudhoofu mwili na afya mbaya	Kulaani, odhoofu wa mwili
Familia kutengekea	Malalamiko, kulaumu wengine
Kukosa fedha za mahiutaji ya msingi kama vile tiba, nguo, kulipia sare za shule	Wizi, uzururaji, ombaomba, kutokuwa katika jamii, kupoteza heshima katika jamii
Kutokuwa na uwezo wa kusaidia wengine katika shida	Kuomba omba chakula kutoka kwa jirani na kwa ndugu na jamaa
Upngufu mkubwa katika upatikanaji chakula	Kutokuwa na uhakika wa upatikanaji wa chakula

u Matokeo u

Kuendelea kwa hali ya juu ya Umasikini

X sababu X

Kufishwa kwa rasilmali ya mifugo	Kuusheheza mno mfumo wa jadi wa kusaidiana	Ongezeko katika asilimia ya watu hali duni
Ongezeko la vifo vya mifugo	Kufishwa kwa malisho katika renji pamoja na uzalishaji	Kupungua kwa mbuga za renji na ubora wa malisho
Ongezeko la kupe	Kuhama nyumbu pamoja na mapanuzi ya maeneo nyumbu	Kupungua kwa upatikanaji wa maji
Kuwekewa vikwazo vya uchomaji moto mbugani	Kuwekewa vikwazo kuchungia katika baadhi ya maeneo	

KIELELEZO 2:

UCHAMBUZI WA WENYE MASLAHI:

Mwenye Maslahi□Maslahi□Wanachochangia (leta)□+au-□Kipaumbele□□Wafugaji□Waliolengwa: unawasaidia katika tatizo la umaskini□Mifugo (ng'ombe + mbuzi) mchango wa fedha, kazi, ulinzi wa Mradi□+□1□□Ilaigwanak□Kijadi huhamasisha jamii kuwasaidia wale walio katika matatizo□Husaidia kuhamasisha, kulinda, usimamizi na kutoa ushauri□+□1□□Watu masikini□Waliolengwa – Mradi utawasaidia kujitoa katika umasikini□Kujitolea nguvu za kazi yao katika kazi wanazozimudu□+□1□□Wafugaji walio katika hali ya kuridhisha□Unapunguza tatizo la kutoa misaada kwa wengine masikini□Ng'ombe, mbuzi, kondoo, usimamizi, ufuatiliaji, huchanga fedha na chakula□+□1□□Wafanya biashara□Ulipunguza soko lao la kuuzia mahindi□Huchanga kama sehemu ya jamii□-□5□□Watumishi wa Mradi pamoja na Wataalam wa Mifugo□Wanakuwa na wateja pamoja na soko zuri□Utaalamu, huduma nzuri, usimamizi wa utekelezaji, hufanikisha malengo yaliyopangwa, kuongeza uzalishaji, uhusiano mzuri, ujuzi wa mazingira□+□2□□NCA□Huthamini Wanyama pori zaidi ya wafugaji□□-□5□□□Wanawaona wafugaji kama sehemu ya matumizi mseto ya ardhi ambayo inabidi waunge mkono□Chakula, kudunga kinga kwa mifugo, kudhibiti magonjwa, kutoa utaalamu unapohitajika□-□3□□Wahisani Serekali ya Denmark□Kupunguza umasikini, kuinua hali ya maisha ya watu masikini□Fedha kwa mfuko wa Mradi, utaalamu, usimamizi, Utetezi wa haki zao wafugaji nia njema, uhusiano mzuri□+□2□□Serekali ya Tanzania□Kupunguza umasikini na kuinua hali ya maisha ya watu masikini□Fedha kwa mfuko wa mradi, kutakiana mema, uhusiano mzuri, taratibu na uhalalishaji□□□□
Mafukara□Hawakulengwa na Mradi kwa sababu hawana wowote wa kuwachangia sehemu pacha ya mifugo kama ilivyo katika mpango wa ewoloto□Nguvu-kazi pale mchango kama huo unapohitajika□-□5□□

3.3 Madhumuni ya Maendeleo:

Hii inajumlisha mambo haya matatu:

(a) Kuboresha hali ya maisha ya Wafugaji katika NCA.
(b) Kuongeza uzalishaji wa mifugo yao.
(c) Jamii ya wafugaji inazidi kujiongezea juhudi za kujitegemea na kujiendesha wenyewe katika jumla ya muundo wa taratibu za matumizi ya ardhi na Hifadhi kama ilivyowekwa katika Sheria ya Hifadhi ya 1959.

Mazungumzo kuchunguza yale mambo matatu ya madhumuni ya maendeleo yalifuata ni nini kifanyike ili madhumuni ya maendeleo yafanikishwe. Hii ilihusishwa kutazama kila moja ya mambo matatu kwa undani zaidi kama ifuatavyo:-

(a) Kuboresha hali ya maisha ya wafugaji katika NCA – ambayo itahusisha:-

- Kuwasaidia wale fukara kabisa kujipatia mifugo tena na hivyo kutokana na uzalishaji wa mifugo hiyo kuwa na uwezo wa kujipatia chakula na mahitaji mengine,

- Kuwasaidia wale waliopatiwa mifugo na chakula cha miaka mitatu ili mifugo hiyo iongezeke kufikia kiwango cha kuweza kuipatia familia chakula bila matatizo,

- Kusaidia katika udhibiti wa magonjwa ya mifugo kwa njia za elimu ya magonjwa makuu na njia za kudhibiti, matumizi ya dipu, chanjo na madawa ya matibabu.

- Kuboresha upatikanaji na usafi wa maji, kuwa na maeneo zaidi ya malisho na matofali ya chumvi za kulambwa.

(b) Kuongeza uzalishaji wa makundi ya mifugo ya wafugaji kunahitaji:-

- Udhibiti wa kupe na magonjwa yaletwayo na kupe.

- Kupanua maeneo ya malisho kwa ujenzi wa maeneo ya maji ambayo yatafanya maeneo mengine kutumika kwa malisho ya mifugo.

- Kuongeza huduma za afya ya mifugo ikiwa ni pamoja na hatua za tiba na uzuiaji.

- Kuwapatia wafugaji elimu ya uzuiaji na tiba ya magonjwa ya mifugo.

c) Jamii ya Wafugaji inazidi kujiongezea juhudi za kujitegemea na kujiendesha wenyewe katika jumla ya muundo wa taratibu za matumizi ya ardhi kama ilivyowekwa katika Sheria ya Hifadhi ya 1959. Hii itahusisha yafuatayo:-

- Kupanua mwamko wa wafugaji juu ya haki zao ndani ya Mpango wa Jumla wa Menejimenti ya NCAA kwa mfano katika matumizi ya Menejimenti ya rasilmali katika maeneo, elimu ya Sheria zinazotawala eneo la Hifadhi, kupatiwa mafunzo viongozi wa jamii za Wafugaji, n.k.

- Ushiriki ulio mkamilifu katika jaribio lolote la kutaka kufanya mabadiliko katika Sheria za sasa zinazoitawala NCA.

- Kuboresha uhusiano na ushirikiano kati ya NCA na Wafugaji kwa:-

  (a) Kuimarisha Idara ya Maendeleo ya Jamii,
  (b) Kuimarisha Baraza la Wafugaji,
  (c) Kuimarisha shughuli za NGO,
  Mafunzo katika ujuzi unaosaidia kuongeza uwezo wa wafugaji na kutunza na kuhifadhi mazingira yao na kuimarisha uhuru wao.

4.0 TATHMINI YA UTEKELEZAJI WA MADHUMUNI YA MAENDELEO

Tathmini ya haraka iliyofanywa na Washiriki kuhusu mambo muhimu ya madhumuni ya maendeleo ilionyesha kwamba mawili ya kwanza (kuboresha hali ya maisha ya wafugaji na ile ya mifugo yao) kwa kiwango kikubwa yana utekelezaji wa kuridhisha kutokana na Programu, ikijulikana kuwa kuna baadhi ya sehemu za Mradi bado hazijatengenezewa maandishi yake, katika kuharakisha kufikia lengo. Washiriki walikerwa na jambo la tatu (Jamii ya wafugaji inazidi kujiongezea juhudi ya kujitegemea na kujiendesha wenyewe…) ambalo halijafanyiwa lolote isipokuwa mafunzo ya viongozi. Maendeleo yoyote katika kufaulisha hili la tatu katika utekelezaji, yatahitaji nia njema na ushirikiano kutoka kwa NCA. Washiriki pia wamekuja kufahamu kuwa maswala mengi yaliyokuja katika GMP ya NCA yanakwenda sambamba na mapendekezo katika lengo hili hata hivyo uongozi wa NCA umekuwa wa kusita sana kupiga hatua katika kutekeleza yaliyopendekezwa. Uimarishaji wa Idara ya Maendeleo ya Jamii, kwa mfano, unachukuliwa kama mzaha. Kuna hisia kuwa Idara hiyo

ambayo ni muhimu mno katika uimarishaji wa uhusiano kati ya NCA na jamii ya Wafugaji, imefanywa hafifu, kwa makusudi, katika muda wa miaka mitatu iliyiopita kwa jinsi uwezo wake ulivyopunguzwa. Ahadi ya NCA ya kuimarisha usalama katika eneo la Kakesio ili kuongeza upatikanaji wa maji na kuwezesha Wafugaji kupeleka mifugo katika maeneo hayo bado haijatimizwa hadi leo.

Hatua ya kwanza ya kuongeza mwamko miongoni mwa wafugaji juu ya haki zao ingelikuwa kwa NCA kutafsiri GMP katika lugha ya Kiswahili na kuendesha warsha katika jamii zote kwa vikundi mbali mbali vikiwepo pamoja na vikundi vya wanawake. Jinsi ilivyotungwa sasa, Idara ya Maendeleo ya Jamii inaonekana kuwa dhaifu mno na kutishwa na Wakuu kiasi kwamba haiwezi kufanya kazi hii muhimu. Baadhi ya Ma-NGO ambazo zinaanza anza kadhalika nazo zinaonekana kugandamizwa kwa hila kwa kupitia Baraza la Wafugaji kiasi kwamba hadi sasa zaidi ya usajili wameshindwa kupiga hatua yoyote katika kushughulikia kazi za jamii. Kwa vile mchango wao kama mashirika ya vyama vya kiraia ni wa muhimu sana katika kusaidia maendeleo ya jamii ya wafugaji, kutokuwepo kwao kunaacha pengo kubwa ambalo haitazamiwi kuwa litaweza kujazwa na mashirika ya kiserikali. Wanayoshughuli nyingine muhimu zaidi ya kuwasaidia wafugaji waweze kufikia lengo la mwisho la madhumuni la kujitegemea na kujiendesha wenyewe.

Ilipendekezwa kuwa programu ingeweza kusaidia kutafsiri GMP hasa zile sehemu zinazohusika na maendeleo ya jamii, kwa ufupisho katika lugha nyepesi ambayo Wafugaji wataweza kusoma na kuelewa. Idara ya Maendeleo ya Jamii katika NCA yaweza kutumia tafsiri hiyo iliyofupishwa kushawishi mwamko wa jamii, na endapo wanasita sita, ma-NGO wanaweza kufanya shughuli hiyo.

UTEKELEZAJI WA MAENDELEZI YANAYOPENDEKEZWA KUHUSU MALENGO YA SASA HIVI

Washiriki waliyatazama tena malengo matano ya muda mfupi ya programu na waliona maeneo yaliyowatia wasiwasi ambayo yanahitaji kuangaliwa katika upangaji wa Awamu ya Pili au ikiwezekana hata zaidi ya hapo. Yafuatayo ndiyo yaliyojitokeza kuhusu kila moja ya malengo ya muda mfupi:-

(a) Upunguzaji wa umasikini na kuboresha hali ya maisha ya Wamaasai wa NCA kwa kuimarisha vyama vya Wafugaji na kwa kuupa msukumo zaidi mfumo wa jadi wa wa Ewoloto wa kusaidiana:

1. Ilionekana japokuwa idadi ya watu fukara sana katika eneo la Mradi ni kubwa, uamuzi na kulenga msaada kwa watu 3,400 tu ulitokana na ugumu wa kupata michango pacha ya mifugo kutoka kwa jamaa wa koo kwa njia ya Ewoloto. Ilipendekezwa kuwa inapowezekana mradi ujaribu kuwasaidia wale masikini sana, pale ambapo Ma-Laigwanak wameweza kushawishi wana jamii kutoa michango pacha.

• Ilionekana kwamba kuna baadhi ya kata ambazo zimekwisha weza kuwasaidia watu 200 zaidi. Mradi unaweza kufikiria uwezekano wa kutoa msaada ama katika awamu hii au katika awamu ijayo ili kuhamasisha msaada kwa familia zingine masikini.

• Ilionekana kwamba mradi umefanya vizuri kuzisaidia familia ambazo hazijapewa mifugo na chakula.

2. Zichukuliwe hatua za kupunguza ucheleweshaji na ugawaji wa chakula usioaminika kwa kuwa na matokeo ya kinyume ya kuzifanya familia zilizolengwa kutokuwa na njia nyingine isipokuwa kuuza mifugo yao ili wajinunulie chakula.

• Ilipendekezwa kuwa kamati za Ewoloto katika kila Kata zihusike katika ufuatiliaji kwa kuunda kamati ndogo yenye wawakilishi kutoka kila Kata. Kamati hiyo itasaidiwa na Eroto.

• Kuhusu ununuzi na ugawaji wa chakula, NCA itaombwa iboreshe mipango na taratibu zake ambazo si hafifu na zenye uhakika.

(b) Huduma za mifugo ziendeshwazo kibinafsi:

1. Ingawa huduma za mifugo za binafsi zilikuwa zimeanza vizuri, katika maeneo mengine huduma zimedhoofu kadiri mahitaji yalivyoongezeka kutokana na familia zaidi kupata mifugo kutokana na mpango wa ewoloto.

Watumishi wa Mradi wameona kuwa bajeti ya kufikia kila familia na kutoa tiba kwa mifugo ni mara 6 kwa mwaka. Kwa kawaida familia nyingi zimeomba kufikiwa mara nyingi zaidi, kiasi kwamba hii imehitaji mafuta zaidi na madawa ya tiba zaidi.

Kuna haja ya kutafakari jinsi gani Mradi utamudu ongezeko la huduma zinazohitajika katika familia zilizolengwa

2. Kuna haja ya kuongeza idadi ya makrashi katika maeneo ya malisho ya mifugo ili kupunguza umbali wa kuswaga mifugo na kupata huduma za afya ya mifugo karibu na maeneo hayo.

3. Inapendekezwa kuwa huduma za dipu ziwe kwenye maeneo yenye maji na pampu za kunyunyuzia dawa za kuua kupe zitumike katika maeneo yasiyo na maji. Wastani wa pampu 5 zinatosha kwa kitongoji kimoja.

4. Magari ya usafiri kwa ajili ya Maofisa wa mifugo yapaswa kuimarishwa ili kuwe na usafiri hasa msimu wa mvua na kuwakinga na hatari za wanyama pori. Inapendekezwa kuwa kila moja ya Kanda tatu iwe na gari yenye uwezo wa kutumika katika mazingira hayo (4-wheel drive). Magari hayo yawe aina ya Suzuki.

5. Ili kuwe na udumishaji wa huduma, Mradi ungelifikiria kuwasaidia maofisa wa mifugo kupewa mtaji wa kuwawezesha kuwa na shughuli hiyo kibinafsi.

(c) Ukarabati wa Maji kwa mahitaji ya wafugaji na mifugo na ujenzi wa vituo vipya uanze, Menejimenti bora ya mbuga za malisho pamoja na uchomaji moto unaodhibitiwa uanze kutumika.

1. Mradi unahitaji kuangalia tena ya maeneo ya baadhi ya Miradi ya maji ambayo ujenzi wake unafikiriwa kwa kutilia maanani maoni ya vikundi vilivyolengwa ili kuhakikisha wote wanafaidika vy ema zaidi. Palipo bwawa la Ntepes kwa mfano, panahitaji kutazamwa tena kutokana na madai kuwa litakuwa na manufaa zaidi kwa wanyama pori kuliko kwa wafugaji. Mradi wa maji wa Orbulati pia wahitaji kuangaliwa upya kwa kuchukulia wasiwasi wa wanawake kuhusu kama mahali hapo ndipo panapofaa. Ilikubaliwa kwamba Mradi utafanya mazungumzo na wafaidi Mradi katika kila eneo, kunyoosha tofauti zozote baina yao kuhusu maeneo hayo.

2. Programu yahitaji kuboresha vyanzo vya maji katika maeneo ambayo kwa sasa hivi hayakaliwi ili kuwezesha maeneo kutumika kwa malisho ya mifugo. Uendelezaji wa vyanzo vya maji umependekezwa katika maeneo yafuatavyo:-

- Kakesio - bwawa liwe Sotuni
- Endulen - bwawa liwe Im'gina
- Oloirobi - bwawa katika Orkiu na Irmunai, Lukumai na Malanja.
- Nainukanuka - bwawa katika Embulbul, Inaasira, Naibor ajijik, Irkiragarie; pampu katika Naipang'pang', bomba la maji katikia Orbulati.
- Naiyobi - bwawa katika Mapenjiro, Iltulele, Engisiwsiw; bomba la maji katika

Engopironi, Olchoro, Engutoto
Ormisigiyo.

- Olbalbal - bwawa katika Nogola na pampu ya maji - Ngololа.

3. Ilionekana kuwa Programu yahitaji kushirikisha NCA katika upatikanaji maji kwa jamii za wafugaji kwa kuwa NCA ina wajibu wa kuboresha huduma hiyo kwa jamii kama ilivyo katika GMP.

(d) Maendelezi ya vikundi vya wanawake katika usagaji wa nafaka na shughuli zing ine kama ufugaji wa wanyama wadogo, utengenezaji wa samli na jibini wakati wa masika ambapo kuna maziwa zaidi ya mahitaji; kushiriki kwa wanawake katika maamuzi ya shughuli za mradi kuimarishwa.

Mradi bado hautoi msaada kwa vikundi vya wanawake ingawa kuna vikundi ambayo tayari vimeishaanzishwa. Vikundi ambavyo vimeishaanzishwa vinangojea msaada kwa shauku kubwa sana.

Matayarisho yafuatayo yanahitaji kuandaliwa ili kuwa tayari kwa programu kuanza:-

- Mafunzo yanahitajika kwa viongozi wa vikundi vya wanawake katika uongozi, utunzaji wa daftari, ujuzi maalum katika baadhi ya shughuli za Mradi, Menejimenti ya Mradi, haki za wanawake wa wafugaji katika jamii, n.k.

- Mradi unahitaji kufuatilia shughuli za vikundi vya wanawake na kupata taarifa kila mwezi.

- Washiriki wa mkutano huu wanahitaji kurudi na matokeo kwa kila jamii kuhusu uanzilishaji wa vikundi vya wanawake.

Ni muhimu kuhakikisha kuwa wanawake wanahusishwa katika kamati kama ifuatavyo:-

- Kamati ya Ewoloto, Kamati ya maji, kamati ya Mradi wa Eroto.

- Kamati ya afya mifugo, Kamati za uwagaji wa chakula.

- Uwezekano wowote wa kuwa na mwanamke kuajiriwa katika kila Kata ungelisaidia sana kuhusisha wanawake katika upitishaji wa maamuzi katika kiwango cha Kata ndani mwa Mradi.

- Kutoa mafunzo ya uongozi kwa wanawake 3 kutoka kila Kata (jumla ya wanawake 18).

(d) Kuwa na kitengo cha kufuatilia uchumi na jamii (Socio-economic, Monitoring Unit) ndani ya NCAA ambayo shughuli yake ni kuimarisha idara ya maendeleo ya jamii ndani ya NCA.

a. Washiriki walieleza kuwa kulikuwa na wakati ambao Idara ya Maendeleo ya Jamii (DCD) ilikuwa ikijishughulisha sana na shughuli za jamii – kuvitembelea vikundi na kuvisaidia moja kwa moja na wengine kubahatika kwenda n g'ambo kwa muda mfupi, jambo ambalo lilisaidia kupanua mawazo yao. Vugu vugu hiyo ilidumu kwa muda mfupi sana.

b. Idara ya Maendeleo ya Jamii ya NCA haitembelei tena jamiii mara kwa mara kutaka kujua matatizo yao na kuweza kutoa msaada na ushauri.

c. Ilipendekezwa kuwa Idara ya Maendeleo ya Jamii (DCD) iimarishwe ili iweze kusaidia kazi za maendeleo ya jamii.

d. Mapendekezo mengine yalikuwa DCD ishirikiane na jamii kwa kufanya kazi kwa ukaribu sana na wanakamati waliochauliwa katika kiwango cha Kata.

e. Washiriki walikerwa kuona kuwa shughuli za Baraza la Wafugaji zimechanganywa kwa makusudi na shughuli za DCD. Hii imeifanya Idara kushindwa kutekeleza wajibu wake. Ilipendekezwa kuwa mwenyekiti wa Ilaigwanak alifuatilie suala hilo kwa NCA na kuleta jibu katika mkutano wa Ilaigwanak unaofuata.

f. Washiriki pia walikerwa na ufanya kazi wa Baraza la Wafugaji ambao umekuwa mdogo na mawasiliano hafifu kati ya wawakilishi wa Kata na wafugaji katika ngazi za jamii, jamii ambayo ndiyo iliyowapa madaraka. Ilionekana kuwa hiyo ni dalili ya uwezo wa kuelewa kuwa mdogo kwa upande

wa Baraza hilo na hivyo ikapendekezwa Mradi kulisaidia kuongeza uwezo wake.

g. Kwa jinsi uwajibikaji wa Baraza la Wafugaji kwa Wafugaji na viongozi wao wa jadi Ilaigwanak, waliowapa madaraka hayo, huonekana kuwa hafifu sana, mkutano uliwaomba Ma-ilaigwanak kufanya ufuatiliaji na Baraza la Wafugaji.

h. Ilifikiriwa kuwa viongozi wa Ma-NGO wangeweza kuleta maoni mapya n awangekuwa wa msaada kama watajiung ana Baraza la Wafugaji. Hata hivyo ilionekana kuwa hii inaweza kuwa ngumu iwapo uanachama wa baraza la wafugaji unafuata Katiba.

6.0 VIELEKEZO (VIDOKEZO):

Washiriki walizungumzia vielekezo ambavyo vitakuwa vya maana kwao katika kupima lengo la maendeleo katika muda mrefu. Vielekezo pia vinaonyesha kama programu itakuwa imeacha ishara. Mdahalo ulizaa mawazo mengi na machache kati yao y ataweza kuchukuliwa kama vielekezo vinavyofaa kwa awamu ya pili baada ya kuchujwa ili yawe SMART: (Specific Measurable Achievable, Realistic and Timebound) yakipekee, yanaweze kupimwa, yanaweza kutimizwa, yenye ukweli na ya katika mabano ya muda.

6.1 Madhumuni ya Maendeleo:

Vielekezo vimewekwa kwa kila moja ya sehemu tatu za madhumuni ya maendeleo kama ifuatavyo:-

(a) Upatikanaji wa Chakula:

- Familia zilizolengwa zinaweza kujipatia chakula chao wenyewe sasa.
- Umbali wa kufikia kwenye maji umefupishwa kiasi kwamba sasa wanaweza kuwatumia watoto kuchota maji.
- Mambo ya familia zilizolengwa kuomba chakula kutoka kwa familia zingine yamepungua sana.
- Afya ya watoto wadogo na watu wazima zimeboreka.

(b) Kuongezeka kwa Uzalishaji wa Mifugo:

- Kuongezeka kwa idadi ya ndama na watoto wa mbuzi

kutokana kwa kasi ya vifo kupungua.

- Waliolengwa kuwa na muda zaidi kuchunga mifugo, kuimarisha maboma ya mifugo na kuwapiga chapa mifugo yao.

- Hakuna tatizo la upatikanaji wa samadi kwa ajili ya kusiriba nyumba na upatikanaji wa ngozi kwa kujengea maboma imara ya ng'ombe. Hii itawawezesha wanafamilia kuwa na muda mwingi zaidi wa kujishughulisha na mifugo kama vile kwenda machungani au kuwaangalia ndama, vitoto vya mbuzi na kondoo katika maeneo ya boma.

c) Jamii ya Wafugaji zinazidi kuendelea kujitegemea na kujiendeshea shughul zao wenyewe.

- Kuongezeka kwa idadi ya mikutano ya wafugaji na ya maamuzi ya masuala yanayowahusu wao.

- Kuongezeka kwa mwamko wa Wafugaji kuhusu haki zao kama ilivyowekwa katika Sheria ya 1959 na kufafanuliwa zaidi katika GMP na kuongezeka kwa kuchukua hatua za kuzidai.

- Uongozi wa vyama mbali mbali vilivyosajiliwa kihalali vinatengeneza kwa uhuru wao mipango ya jamii kwa maendeleo yao wenyewe bila ya kubugudhiwa na NCA.

- Baraza la Wafugaji, Kamati ya Mradi – Eroto na Baraza la Malaigwanak zote zimefanya kazi kwa kushirikiana kusaidia juhudi za jamii za maendeleo.

- Mradi unachangia juhudi za Ma-NGO za kuongeza mwamko wa jamii na kusaidia maendeleo yao.

- Shughuli zinazosaidiwa na Ma-NGO yanayojitokeza katika jamii ya wafugaji kama vile NPA, NGORADEO na NMA zinaongezeka ikionyesha kuongezeka kwa uwezo wao.

- Vikundi vingine vya kujitolea vinavyosaidia huduma za maendeleo katika jamii kama vile kamati za maji, vikundi vya wanawake, haki za wafugaji, n.k.

vinakuwa imara zaidi kutokana na kutambuliwa na kuheshimiwa kwao vyema zaidi.

6.2 **Madhumuni ya Mradi kwa sasa hivi:**

Washiriki walizungumzia vidokezo ambavyo vitakuwa na maana kwa upimaji wa ufanisi wa madhumuni ya sasa. Baadhi ya haya yanaweza kuchujwa zaidi na kupewa mahali pa kutumiwa katika awamu ya pili. Vidokezo vimeendelezwa kwa kila madhumuni kama ifuatavyo:-

(a) Kupunguza umasikini na kuboresha hali ya maisha ya Wamaasai wa NCA kutokana na uimarishwaji wa vyama vya wafugaji na kuwa vuguvugu tena kuhusu taratibu za jadi za kusaidiana iitwayo ewoloto.

Walengwa kwa kila mojawapo kuwa na mifugo mingi zaidi (ng'ombe, mbuzi, kondoo).

- Hawategemei tena misada ya chakula kutoka kwa majirani au marafiki.
- Kujipatia ongezeko la chakula ku tokana na nafsi yake mwenyewe.
- Mtu binafsi (mwanaume) atapendelea zaidi kwenda kuchunga mifugo yake nyakati za mchana.
- Atakuwa na ndama na watoto wa mbuzi nje ya boma
- Watoto na watu wazima watakuwa na afya njema.
- Kumangamanga na kuzurura kunakwisha
- Wizi wa vitu vidogo vidogo kama chakula unakwisha.
- Wanawake wataacha kuomba samadi ya kusiriba nyumba.
- Chokochoko zisizo muhimu na kutengana katika familia hupungua.
- Urahisi wa kupata mkopo kwa sababu ya urahisi na uwezo wa kulipa.

Idadi ya marafiki inaongezeka na heshima inazidi kupanda.

- Husikii tena watu wakizungukazunguka katika jitihada za kutaka kubadilisha watoto kwa mifugo.

(b) Huduma za mifugo zinazoendeshwa kibinafsi zaanzishwa.

- Kupungua kwa vifo vya mifugo wanaopata huduma za afya ikilinganishwa na wale mifugo ambao hawapatiwi huduma hizo.

• Kuongezeka kwa idadi ya mifugo wanaotolewa chini ya utaratibu wa ewoloto.

• Kuelewa zaidi kwa wafugaji juu ya faida za tiba za mifugo.

• Wafugaji hununua dawa za mifugo wenyewe baada ya bajeti inayopangwa na Mradi kwisha.

• Wafugaji waliopata mafunzo kutoka kwa maofisa wa mifugo wana ujuzi na wanaendelea kutoa huduma za afya ya mifugo katika maeneo yao.

Huduma za maji kwa binadamu na mifugo zimekarabatiwa na ujenzi wa vituo viya vya maji umeanza; utunzaji bora wa mbuga za malisho ya mifugo na uchomaji majani wa kudhibitiwa imeanzishwa.

• Mabwawa na mabomba ya maji yanatoa maji ya kutosheleza.

• Vituo vya maji vimejengewa wigo kwa sababu ya ulinzi.

• Umbali wa kutembea hadi maeneo ya maji umepunguzwa sana na wanawake wanatumia muda mfupi zaidi kuchota maji.

• Msongamano wa mifugo katika eneo moja umepungua kutokana kuwa kuna maeneo mengi ya malisho yenye maji.

• Kuna ongezeko la usafi miongoni mwa watoto na watu wazima na hata usafi wa nguo zao na pia hata maradhi ya ngozi ya mwili yatokananyo na kutokuwa wasafi.

• Wanafunzi hutakiwa mara chache zaidi na walimu wao kuja na maji kutoka majumbani mwao au mbali, na ni mara chache walimu kuomba kuletewa maji kwa gari la maji (bowzer).

(d) Maendelezi ya vikundi vya wanawake katika usagaji wa nafaka na shughuli zingine kama ufugaji wa wanyama wadogo, utengenezaji wa samli na jibini wakati wa masika ambapo kuna maziwa zaidi ya mahitaji, hali ya wanawake kuhusu maamuzi ya shughuli za Mradi inahitaji kuimarishwa.

- Michango ya shule na mahitaji mengine ya shule kuweza kutolewa na walengwa.

- Kuongezeka kwa uwezo wa vikundi kuwasaida wengine wakati wa kuzaa, shamrashamra au matatizo yoyote makubwa.

- Uwezo wa kununua chakula kuongezeka.
- Uwezo wa kunua mbuzi au vifaa vingine vinavyoonekana.
- Kikundi kukaa katika hali ya umoja wao kwa muda mrefu zaidi.
- Kuongezeka kwa uwezo wa wanachama kununua nguo.
- Mvutiko kwa watu wengine zaidi kujiunga na kikundi.

Ufanisi wa Idara ya Maendeleo ya Jamiii kuimarika.

- Mpango wa utoaji wa huduma kwa jamii katika eneo la Mradi katika mwaka wa fedha 2001 umemalizika na kupitishwa.
- Matatizo ambayo yamejidhihirisha kwa Ma-ilaigwanak kupitia kwa kamati za Kata, yamepata ufumbuzi.
- Jamii yaridhika kuwa uhusiano na NCA umekuwa mzuri.
- Wizi wa mifugo na makabila jirani umepungua kwa kiasi kikubwa.
- NCA na uongozi wa jadi wapange pamoja njia za kuhakikisha kwamba uonevu na ukandamizaji wa wafugaji unakomeshwa.

Uwezo wa Taasisi za wenyeji kuimarika.

- Taasisi tatu za wenyejji: Baraza la Wafugaji, Washiriki wa Warsha ya Kupeana Habari katika Mradi wa Eroto na Uongozi wa Jadi wa Ma-ilaigwanak wanafanya kazi pamoja kwa lengo moja.
- Shughuli za Mradi zimefaulu na madhumuni kwenye sehemu mbali mbali za Ewoloto, maji, afya ya mifugo na vikundi vya wanawake yamekamilika.
- Bajeti ya Baraza la wafugaji kutoka kwa NCA imeongezeka na kuzifikia taasisi zote tatu.
- Wafugaji wanasikilizwa na haki zao zinaheshimiwa.
- Matatizo ya msingi ya wafugaji yanashughulikiwa kikamilifu
- Shughuli za programu zinapanuka na wahisani wanatoa msaada.
- Haki za wafugaji kutumia kikamilifu mali asili ya eneo la Hifadhi

inatambulika na kukubalika.

- Wafugaji wamedai haki zao ndani ya eneo la Hifadhi na haki hizo wamepewa.

- Taasisi za wenyeji zinatambuliwa kisheria.